Hadithi Ya Mafanikio Katika Ujenzi kwa Ufanisi

Mradi wa Maboresho wa Mahkama Zanzibar (Zi-JUMP) Umeweka Kiwango Kipya Ujenzi wa Majengo 6 ya Mahkama Kupewa Cheti cha Ubora Baada ya Kukidhi Viwango vya Ufanisi wa Hali ya Juu -EDGE (Excellence in Design for Greater Efficiencies).

Mahkama ya Zanzibar (JoZ), kupitia Zi-JUMP, inatekeleza mradi wa kuboresha miundombinu ya mahkama katika visiwa hivyo. Lengo la mpango huu ni kuboresha upatikanaji wa haki, huku ikiboresha majengo ya mahakama ili yawe yenye ufanisi, yanayostahimili mabadiliko ya tabianchi, yenye kufikika kwa urahisi na kuhifadhi mazingira. Zaidi ya hayo, Mahkama ya Zanzibar ililenga kuongeza ufanisi wa mahakama kwa kuwezesha wafanyakazi kitaaluma, na kuboresha Mfumo wa Taarifa wa Mahkama (JIMS) kuwa wa kidijitali ili kuharakisha uendeshajii wa kesi na kupunguza mrundikano wa kesi. Vilevile, kupitia Zi-JUMP, Mahkama ya Zanzibar imelenga kuimarisha ushirikiano wa wananchi na wadau katika sekta ya haki kwa ujumla.



Jengo la Mahkama ya huduma jumuishi lililokidhi viwango vya EDGE . Cheti cha kukidhi viwango vya EDGE kwa jingo la Mahkama ya huduma Jumuishi Mwezi February 2026

Wakati mradi huo ulipoanza hatua ya kubuni michoro ya majengo mwaka 2024, kutumia viwango vya kimataifa vya ujenzi wa majengo yanayohifadhi mazingira (green-building) kwenye majengo ya mahkama na ya serikali ilikuwa namna mpya kabisa kwa Mahkama ya Zanzibar. Viwango vya Ubora wa Michoro ya ujenzi kwa Kuzingatia Ufanisi wa hali ya Juu (EDGE—Excellence in Design for Greater Efficiencies)—ni mfumo wa kimataifa wa utoaji wa vyeti vya ujenzi wa majengo yanayozingatia uhifadhi wa mazingira ulioandaliwa na Shirika la Kimataifa la Fedha (IFC). Unahitaji miradi kuonyesha angalau asilimia 20 ya akiba inayotarajiwa katika matumizi ya nishati, matumizi ya maji, na nishati iliyomo au kaboni katika vifaa vya ujenzi, ikilinganishwa na jengo la kawaida la nchi husika (Zanzibar-Tanzania). Ii kukidhi kiwango cha juu cha EDGE unahitaji angalau asilimia 40 ya akiba ya nishati, pamoja na kizingiti kiwango cha chini cha asilimia 20 kwa maji na vifaa vya ujenzi.

Hapakuwa na hata mmoja wetu aliekuwa na uelewa kuhusu viwango hivyo vya ujenzi si Mahkama zya Zanzibar, , wala Mshauri elekezi (Hab Consult Ltd), wote wawili hawakuwahi kujenga majengo ya umma au binafsi yanayokidhi vigezo vya EDGE. Maarifa na ujuzi wa kubuni majengo vigezo hivyo hatukua nao kufikia viwango vinavyohitajika kwa ajili ya upatikanaji wa cheti cha EDGE. Baada ya kuboresha kwa kina ubunifu kwenye michoro ya ujenzi, na ushauri wa kiufundi kuhusu EDGE kutoka kampuni ya Urban Green Consultants Ltd (UGC) na Mshauri elekezi Hab Consult Ltd, majengo matano yanayojengwa hivi sasa yalipata Cheti cha Awali cha michoro ya ujenzi inayokidhi viwango vya EDGE ila jingo la huduma jumuishi la Tunguu limepata Cheti cha juu cha awali cha EDGE mwezi Februari 2026 hivyo jumla kuwa majengo 6 yenye cheti cha EDGE. Vyeti hivyo vilitolewa na kampuni ya kujitegemea inayojulikana kwa jina la Sintali kulingana na taratibu za tathmini za EDGE.

Katika majengo matano yanayojengwa sasa, mradi unatarajiwa kuokoa kiwango kikubwa ya rasilimali kila mwaka kwa ujumla: Mradi utaokoa matumizi ya umeme ya megawati- 734 kwa mwaka, utaokoa matumizi ya maji ya mita za ujazo 7,459.4 kwa mwaka, na utaokoa kiwango cha kaboni ya tani 1,274.9 isiingie kwenye anga la Dunia kutokana na vifaa vya ujenzi vitakavyotumika. Kwa kutumia dhana zinazolinganisha matumizi ya kaya kupitia utafiti, kiwango cha nishati kitakacho okolewa kila mwaka kitalingana na matumizi ya umeme ya takriban kaya 432 za Zanzibar.[1] Maji yatakayo okolewa katika matumizi ya majengo hayo italingana na matumizi ya maji ya kila mwaka ya takriban kaya 65 hadi 76[2]. Kiwango cha kaboni itakayo okolewa

[1](https://documents1.worldbank.org/curated/en/569391623031256913/txt/Tanzania-Zanzibar-Energy-Sector-Transformation-and-Access-Project.txt

[2] https://openjicareport.jica.go.jp/pdf/11814712_01.pdf

hivyo kutoingia kwenye anga la dunia inakadiriwa kuwa sawa na uwezo wa kufyonza kaboni wa kila mwaka wa miti takriban 57,950 iliyokomaa kutokana na vifaa vya ujenzi vitakavyotumika.[3]

Hata hivyo, jengo la Jendele litakapokamilika, jumla ya majengo itakuwa sita, jambo ambalo litaokoa matumizi ya umeme ya megawati- **849.4 kwa mwaka—sawa na matumizi ya umeme ya kaya 500; kuokoa matumizi ya maji ya mita za ujazo 8,826.2 kwa mwaka—sawa na matumizi ya maji ya kaya 75 hadi 89; na kuokoa kiwango cha kaboni isiingie kwenye anga la Dunia kutokana na vifaa vya ujenzi vinavyotumika tani 1,473.2—sawa na miti 66,964** iliyokomaa ambayo ingehitajika kufyonza kiwango hich cha kaboni. Hii si tu kiwango kikubwa cha nishati kimeokolewa, maji yaliyo okolewa na kaboni iliyozuiliwa isiingie kwenye anga la Dunia, hivyo kutoa mchango mkubwa katika juhudi za kimataifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, bali pia ni punguzo kubwa la gharama za uendeshaji katika majengo hayo ya mahkama yaliyopewa cheti cha EDGE.



Jengo la Mahkama ya Wilaya lililokidhi viwango vya EDGE. *Cheti cha kukidhi viwango vya EDGE kwa jingo la Mahkama ya Wilaya Mwezi Februari 2026*

Jedwali 1: Matokeo ya tathmini ya EDGE kwa kila Jengo

Jengo	Ukubwa wa eneo la chini (m^2)	Kiwango cha nishati katika asilimia kitakacho okolewa kwa mwaka ka	Kiwango cha nishati katika megawati kitakacho okolewa kwa mwaka ka (MWh)	Kiwango cha maji katika asilimia kitakacho okolewa kwa mwaka ka	Kiwango cha maji katika mita za ujazo kitakacho okolewa kwa mwaka (m^3)	Kiwango cha kaboni katika asilimia kitakacho okolewa	Kiwango cha kaboni katika tani za kaboni kitakacho okolewa **(tCO_2e)**
IJC -Tunguu	4,468	45%	272.4	32%	1,992.2	27%	481.4
DMC- Kinduni	1,265	36%	115.6	33%	1,366.8	27%	198.4
DMC- Kijichi	1,265	35%	115.4	33%	1,366.8	22%	198.4
DMC- Makunduchi	1,265	35%	115.5	33%	1,366.8	27%	198.4
DMC- Nungwi	1,265	35%	115.1	33%	1,366.8	27%	198.3
DMC-Jendele	1,265	35%	115.4	33%	1,366.8	22%	198.3
Total	**10,793**		**849.4**		**8,826.2**		**1,473.2**

Mafanikio haya ni muhimu si tu kwa sababu mradi umepata utambuzi wa kimataifa wa ujenzi wa majengo yanayozingatia uhifadhi wa mazingira, bali pia kwa sababu yanaonyesha kuwa uendelevu unaweza kuingizwa katika miundombinu muhimu ya umma, sambamba na utoaji wa huduma zenye ubora wa hali ya juu, kama ilivyothibitishwa katika utafiti wa kuridhika kwa watumiaji wa mahakama Zanzibar wa mwaka 2025, ambapo kiwango cha kuridhika kilikuwa asilimia 80, na sasa Mahakama ya Zanzibar (JoZ) inalenga kuongeza kiwango hicho hadi asilimia 85 ifikapo 2029.

Jaji Mkuu alisema: *"Mahkama ya Zanzibar imeazimia kuhakikisha kuwa upatikanaji wa haki unategemea miundombinu ya kisasa, inayostahimili mabadiliko ya tabianchi na yenye uwajibikaji kwa mazingira. Kupitia Zi-JUMP, tunaonyesha kuwa majengo ya*

[3] catchfoundation.in/blogs/how-many-trees-to-offset-carbon-missions https://share.google/SJHw7BaM7ElNqWZjd

mahkama yanaweza kutoa huduma za haki zenye ubora wa hali ya juu, huku ikiokoa nishati na maji, kupunguza athari za mazingira na kulinda rasilimali za umma kwa vizazi vijavyo. Kwa sasa, utafiti wa kuridhika kwa watumiaji wa huduma za mahkama Zanzibar (2025) umeonyesha kiwango cha kuridhika cha asilimia 80, na tunatarajia kiwango hicho kiongezeke zaidi Insha-Allah".

***Mratibu wa Zi-JUMP alisema**: "Kupata Cheti cha Awali cha ubunifu wa michoro ya ujenzi wa majengo ya mahkama cha EDGE kinaonyesha jitihada na ushirikiano wa timu yote ya mradi. Ilituhitaji kufikiria upya mbinu za kufanikisha, kuimarisha uwezo wa kiufundi na kutumia utendaji unaotegemea ushahidi katika kufanya maamuzi. Matokeo yake ni msingi wa utendajii wa mahkama ambao una ufanisi zaidi, kustahimili mabadiliko ya tabianchi na kukabiliana nayo, na maandalizi mazuri zaidi kwa ajili ya mustakabali wa siku zijazo. Tuko tayari kuendelea kushirikishana uzoefu wetu na hadithi nyingine za mafanikio na kila mtu Tanzania, Afrika na Duniani kote kutokana na kile tulichojifunza hadi sasa katika utekelezaji wa Zi-JUMP. Kwa sasa, Zi-JUMP kwa wastani katika miaka miwili (2024/25 na 2025/26) imefikia shabaha za mradi kwa asilimia 76 katika viashiria vyote 29 (viashiria 10 vya malengo ya maendeleo ya mradi (PDOs) na viashiria 19 vya matokeo ya kati (IRIs). Tunatarajia utendaji wetu ufikie asilimia 90 mwishoni mwa mwaka wa 3 Mei 2027 na angalau asilimia 98 mwishoni mwa mradi Mei 2029 Insha-Allah."*

***Benjamin N. Mtasigwa (Mtaalamu Mwandamizi wa Utawala na Kiongozi wa Mradi (TTL), akiwakilisha Benki ya Dunia) alisema**: "Mradi wa Maboresho wa Mahkama Zanzibar unawakilisha hatua muhimu kama mojawapo ya miradi ya kwanza ya majengo ya mahkama barani Afrika na Afrika Mashariki kupata cheti cha ithibati baada ya kukudhi viwango vya kimataifa vywa ubunifu wa michoro ya ujenzi unaozingatia uhifadhi wa mazingirai vya EDGE kwa majengo ya kisasa ya umma ya mahkama. Mafanikio haya yanaonyesha kuwa miundombinu ya kisasa ya mahkama inaweza wakati huo huo kuboresha upatikanaji wa haki na kusukuma mbele ajenda ya uendelevu wa mazingira. Mradi huu unaweka msingi muhimu wa majengo ya serikali yanayo zingatia uhifadhi wa mazingira Zanzibar na kuwa mfano wa kuigwa wenye thamani kwa taasisi zingine za serikali kuchukua ili kujenga miundombinu ya umma endelevu Tanzania na eneo zima la ukanda huo."*

Kwa taarifa Zaidi wasiliana na:

Mheshimiwa. Aziza I. S. Suewedi (Mratibu wa mradi wa Maboresho ya Mahkama=Zi-JUMP), barua pepe: aziza.suwedi@judiciaryzanzibar.go.tz